

**MATINI YA ELIMU KWA MGONJWA**  
YAMEANDALIWA KWA AJILI YA MATUMIZI YA  
PROGRAMU YA KUBADILI KISUKARI® KWA WATOTO

Jina la kwanza: \_\_\_\_\_

Jina la ukoo: \_\_\_\_\_

Kliniki: \_\_\_\_\_

Taarifa inayotolewa sio mbadala wa ushauri kutoka kwa wataalamu wa huduma ya afya. Wasiliana na daktari au nesi wako kupata ushauri sahihi kuhusu tiba yako.



Matini haya yameandaliwa maalumu kwa ajili ya mpango wa Kubadili Kisukari® kwa Watoto (CDIC). Yanatolewa "kama yaliyyo" na Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH hayatoi warantii ya aina yoyote ile, ikijumuisha – lakini si pekee – warantii zilizodokezwa za kutumika kibishara, uimara kwa lengo fulani bayana au kutovunja utimilifu, usahihii, upatikanaji, ukomo wa muda, utendaji kazi na utifuu wa sheria zinazotumika. Kwa kutumia matini haya unakubaliana na ukweli kwamba taarifa zilizotumika zinaweza zisiwe kamili au sahihi au zinaweza sizitimidile mahitaji au matakwa yako. Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH yanakanusha dhima yoyote ile kwa hasara au uharibifu wa moja kwa moja, usio wa moja kwa moja, utakaojitokeza kwa dharura; andamani, wa adhabu, na wa kipekee; fursa zitakazopotezwa, faida zitakazopotea au hasara nyngine za aina yoyote. Hakimiliki® Novo Nordisk A/S 2012. Haki zote zimehifadihiwa. Si ruhusa kunakili sehemu ya nyaraka hii bilä kibadil cha maandishi kutoka Novo Nordisk A/S.

# 1 Kuchoma insulini ya binadamu



Mwili wangu hautengenezi insulini, nahitaji kuiingiza mwilini kwa kujichoma



1  
Kwanza,  
nanawa  
mikono



Andaa sindano ya insulini, pamba na spiriti



3  
Vingilisha kichupa cha insulini mara 15-20 kati ya mikono yako



4  
Safisha mdomo wa kichupa kwa kutumia spiriti



5  
Safisha sehemu ya kuchoma kwa spiriti



6  
Vuta hewa kwenye bomba la sindano



7  
Ingiza hewa kwenye kichupa cha insulini halafu vuta insulini kwenye bomba la sindano



8  
Hakikisha hakuna hewa kwenye bomba la sindano



Nafinya ngozi yangu na nachoma insulini.



9  
Sutumii sindano tena Naiweka kwenye chupa ya kioo na kuirudisha kliniki.



10  
11

Rudisha kichupa cha insulini kwenye jokofu au sehemu nyingine yenye ubaridi



Kula dakika 30 baada ya kuchoma insulini

# Kuchoma insulini ya binadamu

**Kuchoma insulini ni jambo unalopaswa kulifanyia mazoezi, lakini muda si mrefu utakuwa mzoefu.**

Hizi ni hatua za kufuata:

1. Nawa mikono yako
2. Andaa sindano, pamba na spiriti au kiuu vijidudu kingine
3. Fikicha kichupa cha insulini kati ya mikono yako
4. Safisha kichupa cha insulini kwa spiriti
5. Safisha eneo la kuchoma kwa kutumia spiriti
6. Ingiza hewa kwenye bomba la sindano
7. Vuta insulini kwenye bomba la sindano
8. Hakikisha hakuna hewa kwenye bomba la sindano
9. Choma insulini kwenye sehemu sahihi mwilini mwako (tazama kadi na. 9)
10. Tupa bomba la sindano
11. Rudisha insulini kwenye sehemu baridi
12. Kumbuka kula dakika 30 baada ya kuchoma insulini



Tafuta njia yako kwenye mzingile kwa kufuata hatua za kuchoma insulini katika mpango sahihi



Matini haya yameandalisha maalumu kwa ajili ya mpango wa Kubadili Kisukari® kwa Watoto (CDIC). Yanatolewa "Kama yaliyyo" na Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH hayatoi warantii ya aina yoyote ile, ikijumuisha – lakini si pekee – warantii zilizodokezwa za kutumika kibashara, uimara kwa lengo fulani bayana au kutovunjwa utimilifu, usahihi, upatikanaji, ukomo wa muda, utendaji kazi na utilifu wa sheria zinazotumika. Kwa kutumila matini haya unakuballana na ukweli kwamba taarifa zilizotumika zinaweza zisiwe kamili au sahihi au zinaweza sizitimidilize mahitaji au matakwa yako. Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH yanakusisha dhima yoyote ile kwa hasara au uharibifu wa moja kwa moja, usio wa moja kwa moja, utakaojitekeza kwa dharura; andamani, wa adhabu, na wa kipekee; fursa zitakazopoteza, faida zitakazopoteza au hasara nyingine za aina yoyote. Hakimilikitii® Novo Nordisk A/S 2012. Haki zote zimehifadhiwa. Si ruhusa kunakili sehemu ya nyaraka hii bila kibadli cha maandishi kutoka Novo Nordisk A/S.

## 2 Kwa nini nahitaji insulini


Sote tunahitaji  
nishati kukua  
na kuwa imara



Tunapata nishati  
kutoka kwenye chakula  
tunachokula.



Chakula tunachokula huvunjwa vunjwa  
na kuwa glukosi.



Glukosi inahitaji kuingia seli za mwili wako  
kabla haijatumika kama nishati.

Insulini inafungua milango ya seli za mwili wako,  
ili glukosi iweze kuingia kwenye seli na kutumika



Kama glukosi haiwezi  
kuingia kwenye seli,  
utajisikia kuchoka.



# Kwa nini nahitaji insulini

**Unapokula chakula, mwili wako hubadili sehemu kubwa ya chakula hiki kuwa glukosi (aina ya sukari).**

→ Insulini ni ufunguo unaoruhusu glukosi hii kuingia kwenye seli zote za mwili wako na kutumika kama nishati.

Kama una kisukari, mwili wako hautengenezi insulini ya kutosha au hauwezi kuitumia vizuri, na hivyo glukosi hurundikana kwenye damu yako badala ya kusambazwa na kuingia kwenye seli. Glukosi nyingi sana kwenye damu inaweza kusababisha matatizo makubwa ya kiafya.

Kila mtu mwenye kisukari cha aina ya 1 anahitaji kutumia insulini ili imsaidie kudhibiti viwango vya sukari yao ya damu. Lengo la kutumia insulini ni kuweka kiwango chako cha sukari ya damu katika hali ya kawaida kadiri inavyowezekana na hatimaye ubakie mwenye afya.



## Zungushia jibu sahihi

Tunapata nishati kutoka kwenye:



Chakula tunachokula huvunjwa vunjwa kuwa:



Insulini ni kama:



### 3 Nitumie insulini kiasi gani?



**Ninapaswa kuongeza au kupunguza kiasi cha insulini kufuatana na ninachofanya au ninachokula**

Daktari au nesi wako atakusaidia kufahamu kiasi gani cha insulini uchome kila wakati.



**Punguza au ongeza dozi yako ya insulini kulingana na shughuli unayofanya au unavyojisikia .**



**Zungumza na daktari au nesi wako kuhusu insulini ipi unapaswa kurekebisha, na kwa kiasi gani**

# Nitumie insulini kiasi gani?

**Wakati wote unapaswa kufuata maelekezo ya daktari na nesi wako, lakini wakati mwingine utalazimika kurekebisha kiasi cha insulini mwenyewe.**

Muombe daktari au nesi wako akufundishe wakati gani na kwa kiasi gani urekebishe dozi yako ya insulini.



**Zungushia shughuli zinazoweza kukufanya urekebishe kiasi cha insulini mwenyewe**



## Hali ya kushuka kwa sukari kwenye damu (damusukatiti) na namna ya kuitambua



Kama sukari yangu ya damu itashuka sana, ninaweza kupata hypoglycaemia. Watu wengi wanaiita hali hii kushuka kwa sukari au hipos.



Kutoka jasho



Njaa kali



Kuwashwa midomo



Kuongea kwa shida



Kukereka



Kizunguzungu



Uchovu



Kuona kwa tabu/ukungu



Kulia bila sababu



Kutetemeka



Wakati mwingine kushuka kwa sukari kunaweza kuwa hatari na unaweza kupoteza fahamu au kupata kifafa/degedege

# Hali ya kushuka kwa sukari kwenye damu (damusukatiti) na namna ya kuitambua

**Kushuka kwa sukari kwenye damu kunaweza kuleta madhara – kama itashuka sana, ni hatari zaidi**

Ni rahisi kutambua dalili, lakini inaweza kuwa vigumu kufahamu kama zinatokana na kushuka kwa sukari kwenye damu.

Kumbuka: mara zote unaweza kutumia glukometra kupima kiwango cha sukari kwenye damu.

Unapopata uhakika kuwa dalili hizo zinasababishwa na kushuka kwa sukari kwenye damu, unapaswa kufanya kama inavyoonyeshwa kwenye **kadi na. 6.**

Kumbuka kuwa: watu wanaomzunguka mtu mwenye sukari ya chini ya damu wanapaswa **KUCHUKUA HATUA UPESI!**



**Zungushia dalili za kushuka kwa sukari kwenye damu**



Matini haya yameandaliwa maalumu kwa ajili ya mpango wa Kubadili Kisukari® kwa Watoto (CDIC). Yanatolewa "kama yaliyvo" na Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH hayatoi warantii ya aina yoyote ile, ikijumisha – lakini si pekee – warantii zilizodokezwa za kutumika kibashara, uimara kwa lengo fulani bayana au kutovunja: utimilifu, usahihi, upatikanaji, ukomo wa muda, utendaji kazi na utifu wa sheria zinazotumika. Kwa kutumika matini haya unakubalana na ukweli kwamba taarifa zilizotumika zinawezza zisive kamili au sahihi au zinawezza siziitmilize mahitaji au matakwa yako. Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH yanakunusha dhima yoyote ile kwa hasara au uharibifu wa moja kwa moja, usio wa moja kwa moja, utakaojitekeza kwa dharar; andamani, wa adhabu, na wa kipekee; fursa zitakazopotezwa, faida zitakazopotea au hasara nyngine za aina yoyote. Hakimiliki® Novo Nordisk A/S 2012. Haki zote zimehifadhiwa. Si ruhusa kunakili sehemu ya nyaraka hii bila kibadli cha maandishi kutoka Novo Nordisk A/S.

# 5 Kwa nini ninapata hali ya kushuka kwa sukari kwenye damu (damusukatiti)?

Unapokuwa na kisukari na kutumia insulini kiwango cha sukari yako kwenye damu kinaweza kushuka sana, hali hii inajulikana kama hypoglycaemia.



Sukari yako inaweza kushuka pale:



Unapokuwa umetumia insulini nyingi sana.



Unapokuwa umejichoma sindano ya insulini ya ziada.



Unapokuwa umejishughulisha kupita kiasi na haujarekebia dozi yako ya insulin



Unapokuwa haujala chakula cha kutosha, au umekula mapema sana au umetapika

# Kwa nini ninapata hali ya kushuka kwa sukari kwenye damu (hypoglycaemia)?

changing  
diabetes®  
in children



## Sukari kwenye damu inaweza kushuka kama:

- Umetumia insulini nyingi sana kwa wakati mmoja
- Umechoma sindano ya ziada ya insulini
- Umetumia insulini kama kawaida, lakini baada ya hapo hukula chakula cha kutosha, au umetapika
- Umetumia insulini kama kawaida, lakini umeshughulisha mwili wako kuliko kawaida.

## Zungushia mambo yanayoweza kusababisha sukari yako kwenye damu kushuka



changing  
diabetes™

Matini haya yameandalwa maalumu kwa ajili ya mpango wa Kubadil Kisukari® kwa Watoto (CDIC). Yanatolewa "kama yaliyo" na Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH hayati warantii ya aina yoyote ile, ikijumuisha – lakini si pekee – warantii zilizodokezwa za kutumika kiblashara, uimara kwa lengo fulani bayana au kutovunjwa utimilifu, usahihi, upatikanaji, ukomo wa muda, utendaji kazi na utififi wa sheria zinazotumika. Kwa kutumia matini haya unakubalana na ukweli kwamba taarifa zilizotumika zinaweza zisive kamili au sahihi au zinaweza siziitilizile mahitaji au matakwa yako. Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH yanakanusha dhima yoyote ile kwa hasara au ucharibu wa moja kwa moja, usio wa moja kwa moja, utakaojitezea kwa dharura; andamani, wa adhabu, na wa kipekee; fursa zitakazopoteza, faida zitakazopoteza au hasara nyingine za aina yoyote. Hakimilili© Novo Nordisk A/S 2012. Haki zote zimehifadhiwa. Si ruhusa kunakili sehemu ya nyaraka hii bila kibadil cha maandishi kutoka Novo Nordisk A/S.

ISPAD  
International Society for Pediatric  
and Adolescent Diabetes

Roche


novo nordisk®

# 6 Namna ya kutibu kushuka kwa sukari kwenye damu (hypoglycaemia)



## Kushuka sana kwa sukari kwenye damu

Kama sukari yako kwenye damu imeshuka sana hali yako inaweza kuwa mbaya ghafla na unaweza kupoteza fahamu au "kuzimia"



# Namna ya kutibu hali ya kushuka kwa sukari kwenye damu (hypoglycaemia)

**Wewe, familia yako na marafiki wanapaswa kuchukua hatua UPESI kama utapata dalili za kushuka kwa sukari kwenye damu au hali inaweza kuwa mbaya.**

1. Acha shughuli zote na pumzika.
2. Kula sukari kidogo au kunywa kinywaji chenye sukari au juisi
  - Kama kufanya hivi kutakupa nafuu, unatakiwa kuwa na kitu kigumu cha kula.
  - Kama kufanya hivi hakutakupa nafuu, unapaswa kula sukari zaidi na kupumzika.
  - Kumbuka kutumia glukometa kufanya kipimo cha glukosi kwenye damu kuangalia kama sukari yako imeshuka

Kama sukari yako kwenye damu iko chini sana unapaswa kuharakisha kuwasiliana na daktari au nesi



## Kata majibu yasiyo sahihi

Sukari yako kwenye damu inaposhuka unapaswa:



Kutibu kushuka kwa sukari kwenye damu unapaswa:



Sukari yako ya damu inaposhuka chini SANA unapaswa:



# 7 Baadhi ya aina tofauti za insulini

Insulini zinazofanya kazi haraka



- Inafanya kazi baada ya muda mfupi - dakika 30
- Inaisha nguvu muda mrefu – mpaka masaa 8

Insulin ya NPH:



- Inafanya kazi taratibu - masaa 2
- Inaisha nguvu baada ya muda mrefu – mpaka masaa 18

Insulini mchanganyiko:



- Inafanya kazi baada ya muda mfupi - dakika 30
- Inaisha nguvu baada ya muda mrefu zaidi – mpaka masaa 18

Unaweza kutumia mchanganyiko wa Insulini inayofanya kazi haraka na Insulini ya NPH

Aina za insulini zilizoonyeshwa hapa haziwakilishi aina zote za insulini zilizopo



AU

Insulini mchanganyiko



# Baadhi ya aina tofauti za insulini

Aina tatu za  
insulini ni hizi  
hapa:



## Zinazofanya kazi baada ya muda mfupi:

Insulini hii inafanya kazi haraka sana, lakini hudumu kwa muda mfupi tu. Itaanza kufanya kazi dakika 30 baada ya kuchoma na kudumu kwa saa 8.

## NPH – inafanya kazi taratibu:



Insulini hii huchukua mpaka saa 2 kufanya kazi, lakini nguvu yake itadumu mpaka saa 18.

## Mchanganyiko:

Insulini hii ni mchanganyiko wa insulini za haraka na taratibu. Inachukua mpaka saa 2 kufanya kazi, na itadumu mpaka saa 18.

Aina za insulini zilizoonyeshwa hapa haziwakilishi  
aina zote za insulini zilizopo


## Unganisha mnyama na kichupa sahihi cha insulini:



## 8 Nichome insulini mara ngapi?

Ninapaswa kuchoma insulini kulingana na aina ya insulini ninayotumia.

Daktari au nesi atakusaidia kuamua mara ngapi uchome sindano ya insulini



# Ratiba yangu ya kuchoma insulini

Jina: \_\_\_\_\_  
Tarehe: \_\_\_\_\_

changing  
diabetes®  
in children

## Aina ipi ya insulini nitumie, wakati gani na kiasi gani?



Asubuhi, kabla ya kifungua kinywa

Aina ya insulini: Kiasi gani:



Kabla ya chakula cha jioni

Aina ya insulini: Kiasi gani:



Kabla ya kulala

Aina ya insulini: Kiasi gani:



changing  
diabetes®

Matini haya yameandaliku maalumu kwa ajili ya mpango wa Kubadili Kisukari® kwa Watoto (CDIC). Yanatolewa "kama yalivyo" na Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH hayatoi warantii ya aina yoyote ile, ikijumuisha – lakin si pekee – warantii zilizodekezwa za kutumika kibashara, uimara kwa lengo fulani bayana au kutovunjwa utmilifu, usahihi, upatikanaji, ukomo wa muda, utendaji kazi na utifu wa sheria zinazotumika. Kwa kutumia matini haya unakubaliana na ukweli kwamba taarifa zilizotumika zinaweza zisile kamili au sahihi au zinaweza siziitimilize mahitaji au matakwa yako. Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH yanakanusha dhima yoyote ile kwa hasara au uharibifu wa moja kwa moja, usio wa moja kwa moja, utakaojitokeza kwa dharura; andamani, wa adhabu, na wa kipekee; fursa zitakazopotezwa, faida zitakazopotea au hasara nyalinge za aina yoyote. Hakimiliki© Novo Nordisk A/S 2012. Haki zote zimehifadhiwa. Si ruhusa kunakili sehemu ya nyaraka hili bila kibadil cha maandishi kutoka Novo Nordisk A/S.

ISPAD  
International Society for Pediatric  
and Adolescent Diabetes

Roche

novo nordisk®

# 9 Wapi nichome sindano ya insulini?

Upande wa mbele  
wa mwili wangu kuna sehemu  
tatu ninazoweza kuchoma insulini:

Juu kabisa ya mapaja yangu,  
sehemu ya juu ya mikono  
na kwenye fumbatio.

Hakikisha kuwa kila  
sehemu unayochoma ni  
umbali wa upana wa  
vidole viwili toka sehemu  
uliyochoma mara ya  
mwisho.

Epuka kuchoma karibu  
sana na kitovu.



**Mbele**

**Nyuma**

Upande wa nyuma  
wa mwili wangu kuna  
sehemu moja ninayoweza  
kuchoma insulini:  
sehemu ya juu kabisa ya  
mapaja yangu.

Kumbuka kubadili  
maeneo ya kuchoma



# Wapi nichome sindano ya insulini?

**Insulini inapaswa kuchomwa kwenye tabaka lenye mafuta lililopo chini baada ya ngozi yako.**

Kuna maeneo 4 salama ya kuchoma insulini:

- MAPAJA:** Maeneo ya juu na nje pekee. Usitumie sehemu ya ndani au nyuma ya paja lako.
- MIKONO YA JUU:** Sehemu zenyne nyama kwa pembeni na nyuma ya mikono yako. Epuka misuli ya kwenye mabega.
- FUMBATIO:** Kukatiza kwenye fumbatio lako, kuanzia chini kidogo ya mwisho wa mbavu mpaka chini ya mstari wa mkanda.
- MAPAJA:** Eneo la juu kabisa kwa nje.

**Kumbuka:** kuchoma sindano yako sehemu tofauti kila mara, kuzunguka sehemu zote za mwili wako zilizoainishwa. Kurudia kuchoma sindano sehemu moja mara kwa mara kunaweza kusababisha ngozi kuvimba.




**Zungushia eneo sahihi la kuchoma sindano ya insulini**



# 10 Ninapaswa kula nini?

Nina tengeneza  
piramidi yangu  
kwakushirikiana  
na nesi.



Mboga Za majani



Matunda



Wanga



Na kula zaidi  
vyakula vilivyo  
oneshwa kwenye kundi  
lachini kwenye  
piramidi, nazua kula  
vyakula vilivyo  
oneshwa sahemu ya  
juu ya piramidi.

# Ninapaswa kula chakula cha aina gani?



**Kama una kisukari, chakula unachokula ni muhimu kwa sababu kinachangia namna unavyojisikia na namna insulini inavyofanya kazi.**



- Wewe na familia yako mnaweza kutumia piramidi ya chakula kujua namna ya kuchanganya aina tofauti za vyakula pamoja.
- Kula zaidi vyakula viliwyopo kwenye ukanda wa chini wa piramidi.
- Kula baadhi ya vyakula viliwyopo kwenye ukanda wa kati wa piramidi
- Kula kidogo zaidi kutoka kwenye ukanda wa juu wa piramidi

**Kwa kushirikiana na nesi wako, chora aina ya vyakula unavyokula kwenye piramidi**



# 11 Kupima sukari yangu kwenye damu

Wakati wote unapaswa kufahamu kama una sukari ya juu sana au ya chini sana kwenye damu yako.



Tunakupatia glukometa, utepe, kitabu cha kumbukumbu cha kisukari na Sindano.



ANGALAU  
4 X

Unapaswa kutumia glukometa yako angalau mara 2 kwa siku na kuandika namba/matoke unayopata.



Unapoamka,



Saa 2 baada ya kupata kifungua kinywa.



Jioni, kabla ya chakula cha jioni



Kabla ya kwenda kulala



Kiwango cha afya cha sukari ya damu ni katika ya 4.5 and 10 mmol/l (80 and 180 mg/dl).\*



Siku zote unapaswa kuchukua glukometa yako na kitabu cha kumbukumbu cha kisukari kila unapokwenda kliniki



# Kupima sukari yangu ya damu

**Unahitaji kufahamu kama una sukari nyingi sana au kidogo sana kwenye damu yako.**

**Ni vyema kama utapima sukari yako mara 4 kwa siku kwa kutumia kifaa cha kupimia:**

1. Unapoamka asubuhi
2. Saa 2 baada ya kupata kifungua kinywa.
3. Jioni kabla ya kula chakula cha jioni
4. Kabla ya kwenda kulala.

**Unapaswa kuandika matokeo/namba hizi kwenye kitabu chako cha kumbukumbu cha kisukari.**

Wakati wote chukua kitabu chako cha kumbukumbu cha kisukari unapokwenda kliniki. Namba itakuwa juu mara baada ya milo au kama ulikuwa na hasira au kuumwa. Itakuwa chini baada ya kufanya mazoezi ya mwili au shughuli nzito.

**Kufuatilia sukari yako kwenye damu kutakusaidia kujisikia vizuri.**

**Zungushia vitu unavyohitaji kupima hali ya sukari yako kwenye damu**



Matini haya yameandalwa maalumu kwa ajili ya mpango wa Kubadil Kisukari® kwa Watoto (CDiC). Yanatolewa "kama yaliyo" na Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH hayatol warantii ya aina yoyote ile, ikijumuisha – lakini si pekee – warantii zilizodokezwa za kutumika kibashara, uimara kwa lengo fulani bayana au kutowunjwa utimilifu, usahihi, upatikanaji, ukomo wa muda, utendaji kazi na utifu wa sheria zinazotumika. Kwa kutumika matini haya unakuballana na ukweli kwamba taarifa zilizotumika zinaweza zisiwe kamili au sahihi au zinaweza siziitimidile mahitaji au matakwa yako. Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH yanakanusha dhima yoyote ile kwa hasara au uharibifu wa moja kwa moja, usio wa moja kwa moja, utakaojitekeza kwa dharura; andamani, wa adhabu, na wa kipekee, fursa zitakazopeteza, faida zitakazopeteza au hasara nyingine za aina yoyote. Hakimilikit® Novo Nordisk A/S 2012. Haki zote zimehifadhiwa. Si riuhusa kunakili sehemu ya nyaraka hili bila kibadil cha maandishi kutokea Novo Nordisk A/S.

## 12 Ninatumiaje glukometa yangu?



Ili kupima sukari yangu ya damu ninahitaji kuandaa baadhi ya vitu. Ninahitaji: sabuni, kisu kidogo, glukometa, utepe, pamoja na kitabu cha kumbukumbu cha kisukari.



Chini ya sekunde 30 zitakazofuata glukometa itaonyesha namba. Namba hii ndiyo kiwango changu cha sukari ya damu. Ninapaswa kuandika namba hii kwenye kitabu cha kumbukumbu cha kisukari.



Wakati wote ninapaswa kukumbuka kuchukua kitabu changu cha kumbukumbu cha kisukari ninapokwenda kliniki na kumpatia nesi.

Hii itamsaidia na kunisaida pia.



Taarifa inayotolewa sio mbadala wa ushauri kutoka kwa wataalamu wa huduma ya afya. Wasiliana na daktari au nesi wako kupata ushauri sahihi kuhsu tiba yako.

# Ninatumiaje glukometa yangu?

**Kabla ya kupima sukari yako ya damu, unahitaji kuandaa vitu vifuatavyo:**

- Sabuni
- Kifaa cha kukatia na kisu kidogo
- Utepe
- Glukometa

**Kufanya kipimo, fuata hatua zaifuatazo:**

1. Safisha mikono yako
2. Washa glukometa na chomeka utepe ndani
3. Choma kidole chako kwa prika
4. Weka tone la damu kwenye utepe
5. Subiri na usome namba ilioneshwa kwenye glukometa
6. Andika namba kwenye kitabu cha kumbukumbu



**Unganisha hatua za kupima sukari yako kwenye damu kuanzia mwanzo mpaka mwisho**



Matini haya yameandalwa maalum kwa ajili ya mpango wa Kubadili Kisukari® kwa Watoto (CDIC). Yanatolewa "kama yaliyo" na Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH hayatali warantii ya aina yoyote ile, ikjumuisha – lakin si pekee – warantii zilizodokezwa za kutumika kiblashara, uimara kwa lengo fulani bayana au kutovunjwa utimilifu, usahihi, upatikanaji, ukomo wa muda, utendaji kazi na utilifu wa sheria zinazotumika. Kwa kutumia matini haya unakuballana na ukweli kwamba taarifa zilizotumika zinaweza zisiwe kamili au sahili au zinaweza siziitirilize mahitaji au matakwa yako. Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH yanakanusha dhima yoyote ile kwa hasara au uharibifu wa moja kwa moja, usio wa moja kwa moja, utakaojitekeza kwa dharura; andamani, wa adhabu, na wa kipekee; fursa zitakazopoteza, faida zitakazopoteza au hasara nyininge za aina yoyote. Hakimilliki® Novo Nordisk A/S 2012. Haki zote zimehifadhiwa. Si ruhusa kunakili sehemu ya nyaraka hii bila kibadli cha maandishi kutoka Novo Nordisk A/S.

## 13 Hali ya kupanda kwa sukari kwenye damu (damusuziada) na namna ya kuitambua



Kama sukari yanu ya  
damu itapanda sana,  
ninaweza kupata  
hyperglycaemia.

Inawezekana ukawa na sukari ya juu ya  
damu kama:



unasaki kiu muda wote



unajisikia kukojoa sana



Huwezi kuona vizuri



Unajisikia kuchoka muda wote

Kama ni hali mbaya ya kupanda kwa sukari  
ya damu unaweza pia kupata:



kichefuchefu



maumivu ya tumbo



kupumua kusiko kawaida



kutoa hewa inayonukia kama pombe



Angalia kiwango  
chako cha glukosi  
ya damu kuthibitisha  
kama sukari yako  
kwenye damu  
imepanda  
(hyperglycaemia).



Mdomo wako unakauka



kupoteza fahamu



kama unahisi una mojawapo ya  
dalili hizi – nenda kliniki!

# Hali ya kupanda kwa sukari kwenye damu (damusuziada) na namna ya kuitambua

**Kupanda kwa sukari ya damu au hyperglycaemia hutokea pale mwili unapokuwa na insulini kidogo sana au pale mwili unaposhindwa kutumia insulini vizuri.**

Sukari ya damu ambayo iko juu sana inaweza kuwa tatizo kubwa kama hutaitibu, na hivyo ni muhimu kuanza matibabu mapema iwezekanavyo mara tu utakapogundua hali hiyo. Sehemu ya kudhibiti kisukari chako ni kupima glukosi yako ya damu mara kwa mara. Kupima damu yako, na halafu kutibu kupanda kwa sukari mapema kutakusaidia kuepuka matatizo yanayosababishwa na hyperglycaemia.

Kama una mojawapo ya dalili zifuatazo, nenda kamwone daktari haraka:

- Kupumua haraka haraka
- Pumzi yenyé harufu ya pombe
- Kichefuchefu na kutapika
- Mdomo mkavu sana

**Kumbuka kumwambia daktari wako kuwa una kisukari cha aina ya 1 na kwamba sukari yako kwenye damu iko juu sana.**

## Zungushia dalili zote za kupanda sana kwa sukari kwenye damu



Kichefuchefu



Kiu sana muda wote



Kuchoka muda wote



Pumzi yenyé harufu ya pombe



Maumivu ya tumbo



Kutopumua kwa kawaida

14

## Kwa nini napata hali ya kupanda kwa sukari kwenye damu (damusuziada)?

Unapokuwa na kisukari kiwango chako cha sukari kwenye damu kinaweza kupanda sana. Hali hii inajulikana kama hyperglycaemia.



Sukari yako kwenye damu inaweza kupanda kama:



Umetumia insulini kidogo sana au umekosa kuchoma sindano ya insulini.



Umetumia insulini isiyofaa kwa sababu ilikuwa imekaa sana au ilihifadhiwa kimakosa.



Umekula chakula kingi sana.



Hukushughulisha mwili kwa muda mrefu isivyo kawaida.



Una maambukizi au homa.

# Kwa nini napata hali ya kupanda kwa sukari kwenye damu (damusuziada)?



## Sukari yako ya damu inaweza kupanda pale:

- Unapokuwa na insulini kidogo sana au unapokosa kuchoma sindano ya insulini
- Unapokosa kuushughulisha mwili kwa muda mrefu kuliko ilivyo kawaida
- Unapokula chakula kingi kupita kiasi
- Unapotumia insulini isiyofaa kwa sababu ilikuwa imekaa kwa muda mrefu au haikuhifadhiwa kwa usahihi
- Unapokuwa na uambukizo, homa au kidonda cha mguuni

## Zungushia picha za vitu vinavyoweza kusababisha kupanda kwa sukari ya damu



Unapotumia insulini isiyofaa kwa sababu ilikuwa imekaa kwa muda mrefu au haikuhifadhiwa kwa usahihi.



Unapokula chakula kingi kupita kiasi.



Unapotumia insulini nyngi sana kwa wakati mmoja .



Umeshughulisha mwili wako sana kuliko kawaida.



Hukushughulisha mwili wako kwa muda mrefu kuliko ilivyo kawaida.



Umetumia insulini kidogo sana au umekosa kuchoma sindano ya insulini.



Hujala chakula



Unapokuwa na uambukizo, homa



Umechoma dawa ya insulini zaidi ya kiwango

Matini haya yameandalwa maalumu kwa ajili ya mpango wa Kubadil Kisukari® kwa Watoto (CDiC). Yanatolewa "kami yaliyo" na Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH hayatil warantii ya aina yoyote ile, ikijumuisha – lakini si pekee – warantii zilizodokezwa za kutumika kibishashara, ulimara kwa lengo fulani bayana au kutowunjawna utimilifu, usahihi, upatikanaji, ukomo wa muda, utendaji kazi na utifuu wa sheria zinazotumika. Kwa kutumila matini haya unakuballanza na ukweli kwamba taarifa zilizotumika zinaweza zisiwe kamili au sahihi au zinaweza siziitimidilize mahitaji au matakwa yako. Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH yanakanusha dhima yoyote ile kwa hasara au uharibifu wa moja kwa moja, usio wa moja kwa moja, utakaojitekeza kwa dharura; andamani, wa adhabu, na wa kipekee, fursa zitakazopoteza, faida zitakazopoteza au hasara nyingine za aina yoyote. Hakimiliki© Novo Nordisk A/S 2012. Haki zote zimehifadhiwa. Si rufusa kunakili sehemu ya nyaraka hii bila kibadil cha maandishi kutoka Novo Nordisk A/S.

15

## Namna ya kutibu hali ya kupanda kwa sukari kwenye damu (damusuziada)?

changing  
diabetes®  
in children



Kutibu hali ya kupanda kwa sukari kwenye damu unapaswa:



Pima glukosi yako ya damu



Tumia insulini inayofanya kazi haraka



Pima tena glukosi baada ya saa 2 kupita

### KUPANDA KWA SUKARI YA DAMU

Kama glukosi yangu ya damu ni katiki ya 11 na 22 mmol (200 na 400mg/dl)

Wasiliana na daktari au nesi wako kama huna uhakika nini cha kufanya.



- Kama sukari yako ya damu bado ipo juu:
1. rudia dozi ya ziada
  2. wasiliana na daktari au nesi wako



Muulize daktari au nesi wako ni kiasi gani cha nyongeza cha insulini unapaswa kutumia.



**KUMBUKA:** Wakati wote unapaswa kunywa maji mengi.

### KUPANDA SANA KWA SUKARI KWENYE DAMU

Kama glukosi yako kwenye damu ni zaidi ya 22 mmol (400mg/dl)

Unapaswa Kuwasiliana na kliniki upesi!

Ninapaswa kutumia insulinini haraka - 10% ya jumla ya dozi yangu ya siku.



# Namna ya kutibu hali ya kupanda kwa sukari kwenye damu (damusuziada)?

changing  
diabetes®  
in children

Mara nyingi ni rahisi kutibu matukio ya kupanda kwa sukari ya damu (hyperglycaemia):

1. Pima glukosi yako ya damu
2. Tumia insulini
3. Pima glukosi yako ya damu tena baada ya saa mbili.

Unapopima mara ya pili, namba inayoonekana inatakiwa iwe imeshuka

Kama sivyo, unapaswa kuchoma tena sindano ya insulini.

Kama sukari yako ya damu imepanda (zaidi ya 22mmol), unapaswa kumuona daktari au nesi haraka.

Unahitaji msaada wao kutibu matukio ya hatari ya kupanda kwa sukari ya damu.

Hali hiyo haiwezi kutibika nyumbani.



## Zungushia jibu sahihi

Sukari yako ya damu inapopanda, unapaswa:

Kupima glukosi ya damu



Osha miguu



Kama sukari ya damu imepanda sana, unapaswa:

Kwenda shulen



Kumwona daktari au nesi upesi



Matini haya yameandalisha maalumu kwa ajili ya mpango wa Kubadil Kisukari® kwa Watoto (CDIC). Yanatolewa "kama yaliyo" na Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH hayati warantii ya alia yoyote ile, ikijumuisha – lakini si pekee – warantii zilizodokeza za kutumika kibashara, uimara kwa lengo fulani bayana au kutovunja: utimilifu, usahihi, upatikanaji, ukomo wa muda, utendaji kazi in utifu wa sheria zinazotumika. Kwa kutumia matini haya unakuballana na ukweli kwamba taarifa zilizotumika zinawezsi zisive kamili au sahihi au zinawezsizitilizze mahitaji au matakwa yako. Mashirika ya Novo Nordisk A/S na Roche Diagnostics Deutschland GmbH yanakanusha dhirma yoyote ile kwa hasara au uharibifu wa moja kwa moja, usio wa moja kwa moja, utakaojitokeza kwa dharura; andamani, wa adhabu, na wa kipekee; fursa zitakazopoteza, faida zitakazopoteza au hasara nyngine za alia yoyote. Hakimiliki® Novo Nordisk A/S 2012. Haki zote zimehidadihwa. Si ruhusa kunakili sehemu ya nyaraka hili bila kibadli cha maandishi kutoka Novo Nordisk A/S.

changing  
diabetes®

ISPAD  
International Society for Pediatric  
and Adolescent Diabetes

Roche

novo nordisk®

## 16 Kutunza miguu yangu

Ni muhimu  
kutunza miguu  
yangu –  
kutofanya hivyo  
kunaweza  
kusababisha  
magonjwa



Kagua miguu  
yako kuona kama  
kuna: vidonda,  
kujikata, alama  
nyekundu,  
uvimbe na kucha  
zenye uambukizo



Madoa  
mekundu



Osha miguu yako kila siku



LOTION

4

Paka losheni kwenye miguu yako




Weka kucha fupi na safi



Weka miguu yako juu ipumzike



Vaa viatu  
wakati wote



Jishughulishe



Mwombe  
daktari au nesi  
wako akukague  
miguu yako.

# Kutunza miguu yangu


Kama una kisukari unapaswa kuchukua hatua za ziada kutunza miguu yako. La sivyo, miguu yako inaweza kuharibika na unaweza kupoteza kidole, mguu wa chini au hata mguu wote. Kutunza miguu yako vizuri kunaweza kuzuia haya yasitokee.

## Unapaswa:

- Kagua miguu yako kuona kama kuna: vidonda, kujikata, alama nyekundu, uvimbe na kucha zenyе uambukizo
- Osha miguu yako vizuri kila siku, ikaushe na paka losheni
- Weka kucha zako fupi na safi
- Weka miguu yako juu ipumzike
- Wakati wote vaa viatu, lakini hakikisha haviumizi miguu yako na kukupa michubuko
- Jishughulishe
- Mwombe daktari au nesi akagee miguu yako kila uendapo kliniki.



Tafuta njia yako kwenye mzingile ili kufika kwenye miguu yenyе afya na kuepuksana na miguu yenyе vidonda! Hakikisha unapitia vitu vyote vizuri vyta kufanya kwa miguu yako unapokuwa njiani.



## 17 Kuishi na kisukari



Japokuwa nina kisukari, bado ninaweza kushiriki katika shughuli zote za kawaida.



Punguza insulini yako kama utajishughulisha kupita kiasi.



Punguza insulini yako kama utatembea umbali mrefu zaidi ya kawaida



Punguza insulini yako kama utakula chakula kidogo au kutokula kabisa



Ongeza insulinini yako kama unatarajia kula kuliko kawaida



Si mara zote shughuli mbalimbali hupangwa, na kama unajishughulisha kimwi kuliko kawaida bila kupanga basi unapaswa kula chakula au kunywa vimiminika ambavyo vina sukari nyngi.



Wakati wote beba sukari ikusaidie wakati wa kushuka kwa sukari ya damu

# Kuishi na kisukari

Watu wenge kisukari wanaweza kushiriki kwenye shughuli zote za kawaida. Lakini huna budi kubadili (kuongeza au kupunguza) kiasi cha insulini unachotumia kulingana na shughuli unayopanga kuifanya.

- Kama utajishughulisha sana, unapaswa kupunguza kiasi cha insulini unachotumia asubuhi.
- Kama utasafiri au kutembea umbali mrefu, unapaswa pia kupunguza kiasi cha insulini unachotumia.
- Kama utapitisha muda wa kula bila kula, unapaswa kupunguza kiasi cha insulini unachotumia.
- Kama utakula chakula kingi kupika kiasi, unapaswa kuongeza kiasi cha insulini unachotumia.
- Kama unajishughulisha sana na hujabadili kiasi cha insulini unachotumia, unapaswa kula vyakula au kunywa vinywaji vyenye sukari nyingi.
- Kama umeenda mbali na nyumbani kwa zaidi ya saa 6, siku zote hakikisha unabeba dawa, sindano, glukometra na chakula kidogo pamoja na maji.

Chora mshale unaoonyesha juu au chini, kuonyesha namna unavyopaswa kurekebisha kiasi cha insulini unachotumia katika mazingira tofauti.



The Novo Nordisk A/S Bull logo and Changing Diabetes® are registered trademarks owned by Novo Nordisk A/S.

